


Chama Cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu
Website: <http://tthu.biz.tc>



LIJUE CHIMBUKO LA THTU

- Chama (THTU) kimepata usajili wa kudumu Reg. No 23 kilichotolewa na msajili wa vyama tarehe 12 – 12 – 2008 chini ya sheria namba 6 ya Kazi na Mahusiano ya Ajira na sheria No. 7 ya Taasisi za Ajira
- Chimbuko la THTU ni jopo la viongozi wa vyama vya wafanyakazi, wanataaluma na mabaraza ya wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu lililoundwa miaka ya tisini kwa ajili ya kuwasilisha Serikalini na kujadili mapendekezo ya maboresho ya mishahara, mafao ya uzeeni na mazingira kazi
- Jopo hilo lilifanikisha kuongezeka kwa mishahara mwaka 1998 kufuatia juhudi kubwa zilizopelekea serikali iyaafiki mapendekezo ya jopo.
- Mwaka 2005 Jopo lilifanikiwa kuifanya serikali iunde kamati ya Rais ya 2005 iliyopokea mapendekezo saba ya kuboresha mishahara, mafao ya uzeeni, miundo mbinu, vitendea kazi, maslahi mbalimbali, na bajeti za kutosha za maendeleo ya taasisi.
- Kuanzia mwaka 2005 hadi mwanzoni mwa 2008 jopo hilo liliendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya kamati ya Rais ya 2005.
- Baada ya kukwazwa na kauli na vitendo vya chama kilichokuwa na dhamana ya kutetea maslahi ya wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu jopo lilichukua uamuzi wa kusajili chama kipya cha wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu.
- Maamuzi ya Kusajili chama yalifanyika katika mkutano wa viongozi wa tarehe 18 – Feb – 2008 uliofanyika ukumbi wa maktaba chuo Kikuu DSM.
- Pamoja na pingamizi kubwa toka chama kilichokuwepo Serikali iliridhia kusajili chama kipya tarehe 12 – 12 – 2008